

2- الوَقْفُ الكافي Al-Waqf Al-Kaafiy - Kisimamo Cha Kutosheleza

Ni kusimama katika neno la Qur-aan ambalo imetosheleza maana yake, na kuna uhusiano na kauli inayofuatia katika maana lakini hakuna uhusiano kilugha.

Hukmu yake: Inasimamiwa na inaweza kuanziwa.

Mifano ya الوَقْفُ الكافي Al-Waqf Al-Kaafiy - Kisimamo Cha Kutosheleza

- Mfano wa kwanza mwishoni mwa Aayah:

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا سَوَاءٌ عَلَيْهِمْ ءَأَنْذَرْتَهُمْ أَمْ لَمْ تُنذِرْهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٦٧﴾ خَتَمَ اللَّهُ عَلَى قُلُوبِهِمْ

((Hakika wale waliokufuru ni sawa kwao, ukiwaonya au usiwaonye wao hawatoamini)) ((Allaah Amapiga mhuri juu ya nyoyo zao))¹

Aayah ya kwanza hapo inataja kuhusu makafiri kwamba ukiwaonya au usiwaonye hawataamini. Kisha Aayah ya pili yake inaendelea kutaja maudhui hiyo hiyo inayohusu makafiri kwamba **“Allaah Amapiga mhuri juu ya nyoyo zao”**.

Mfano wa pili mwishoni mwa Aayah:

﴿ وَإِنَّ مِنْ شِيعَتِهِ لَإِبْرَاهِيمَ ﴾ إِذْ جَاءَ رَبَّهُ بِقَلْبٍ سَلِيمٍ ﴿٦٨﴾

((Na hakika katika kundi (wafuasi, wenye kwenda mwendo) wake bila shaka ni Ibraahim.)) ((Alipomjia Mola wake kwa moyo saliyim [uliotakasika na shirki, kufuru, unafiki, shubha, matamano, na kusalimika na kila ovu]))²

¹ Al-Baqarah (2: 6-7)

² Asw-Swaffaat (38: 83-84)

Aayah ya kwanza ametajwa Ibraahiym (عليه السلام) ambaye amesifiwa kwamba amefuata mwendo wa Nabii Nuwh (عليه السلام) katika Dini na da'wah yake, ambaye ametangulia kutajwa katika Aayah za nyuma. Aayah hiyo ya kwanza imetosheleza kimaana na kisha Aayah ya pili inaendelea kumuelezea Ibraahiym (عليه السلام).

- Mfano wa kwanza katikati ya Aayah:
Kusimama katika:

رَبَّنَا تَقَبَّلْ مِنَّا

Kisha kuanza kinachoendelea kama ilivyo katika Aayah:

رَبَّنَا تَقَبَّلْ مِنَّا إِنَّكَ أَنْتَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ

((Mola wetu, Takabali kutoka kwetu, hakika Wewe ni *as-Samiy'ul-'Aliym* [Mwenye kusikia yote daima - Mjuzi wa yote daima]))³

- Mfano wa pili katikati ya Aayah:

Unaweza kusimama kwenye neno **ذُكِّرْتُمْ**; pia kwenye neno **مَعَكُمْ** katika kauli yake Allaah (سبحانه وتعالى):

﴿ قَالُوا طَئِيرُكُمْ مَعَكُمْ أَيْنَ ذُكِّرْتُمْ بَلْ أَنْتُمْ قَوْمٌ مُّسْرِفُونَ ﴾

((Mitume) Wakasema: "Nuksi yenu mnayo wenyewe. Je, kwa vile mnakumbushwa? Bali nyinyi ni watu wapindukao mipaka.")⁴

Na kisha kuanza na kinachokuja baada ya hapo uliposimama katika hiyo Aayah. Kwa sababu yaliyotangulia yametoshleza maana na yanahusiana na yanayofuatia katika maana.

³ Al-Baqarah (2: 127)

⁴ Yaasiyn (36: 19)

Mifano miwili mingineyo miongoni mwa mingi katika Qur-aan.

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تُلْهِكُمْ ءَمْوَالُكُمْ وَلَا أَوْلَادُكُمْ عَنْ ذِكْرِ اللَّهِ ؕ وَمَنْ يَفْعَلْ ذَلِكَ
فَأُولَئِكَ هُمُ الْخٰسِرُونَ ﴿٦٦﴾

((Enyi mlioamini! Yasikushughulisheni mali zenu na wala auladi wenu na dhikri⁵ ya Allaah. Na yeyote (yule) atakayefanya hivyo basi hao ndio waliokhasirika.))⁶

الَّذِي خَلَقَ سَبْعَ سَمَوٰتٍ طِبَاقًا ۗ مَا تَرَىٰ فِي خَلْقِ الرَّحْمٰنِ مِن تَفٰوُتٍ ۗ فَارْجِعِ الْبَصَرَ
هَلْ تَرَىٰ مِن فُطُوْرٍ ﴿٦٧﴾

((Ambaye Ameumba mbingu saba matabaka, hutaona katika uumbaji wa *Ar-Rahmaan* (Mwingi wa Rehma) tofauti yoyote. Basi rejsha jicho (mbinguni), je, unaona mpasuko wowote (ule?))⁷

⁵ Kumdhukuru Allaah kwa kila aina; kukumbuka Utukufu Wake, neema Zake, ihsani Yake kwa kutaja jina Lake; kumsabbih, kumpwekesha, kumshukuru, kumsifu, kumtukuzi, kuomba maghfirah, kusoma Qu-raan, kumswalia Mtume (صلى الله عليه وسلم), na kwa kuzingatia na kuyataamali Majina Yake Matukufu.

⁶ Al-Munaafiqun (63: 9)

⁷ Al-Mulk (67: 3)